



East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 6, Issue 2, 2023

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>

EANSO

EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

Tathmini ya Matatizo ya Kiisimu na Kimtindo katika Matini Tafsiri za Kidini: Mfano Wa Njia Salama, Walioteliwa Na Vita Kuu

Vince Arasa Nyabunga^{1*} Dkt. Miriam Osore, PhD¹ na Dkt. Leonard Chacha Mwita, PhD¹

¹ Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.

* Barua pepe ya mawasiliano: vincenyabunga21@gmail.com

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1639>

Tarehe ya Uchapishaji: **IKISIRI**

19 Desemba 2023

Istilahi Muhimu:

*Tafsiri,
Matatizo ya Kiisimu na
Kimtindo.*

Makala haya yalitathmini matatizo ya kiisimu na kimtindo katika vitabu vya kidini: Njia Salama (1977), Walioteuliwa (2009) na Vita Kuu (1952), (White). Lengo la makala hii lilikuwa kutathmini matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini teule na kuonyesha namna yaliathiri uelewaji na ufasiri wa mafunzo tafsiri miongoni mwa waumini wa SDA. Matatizo ya kiisimu yaliyochunguzwa yalikuwa pamoja na ya kisematiki, kisintaksia, na kimofolojia. Nayo ya kimtindo yalikuwa urudiaji, uradidi, na tofauti za kipolisemia. Utafiti huu ulitumia mbinu za kimaelezo na kitakwimu katika kukusanya na kuchanganua data. Nyanjani, sampuli tarajiwa ilikuwa washiriki 140. Kwa hivyo, viongozi 42 na waumini 98 katika makanisa saba ya SDA waliteuliwa na kutoa sampuli ya utafiti. Maktabani, vitabu teule vilisomwa na vifungu vyenye matatizo ya kiisimu na kimtindo viliainishwa, kuteuliwa na kuunda data ya utafiti. Nadharia ya skopos ilitumiwa katika utafiti huu. Nadharia ya skopos, inaeleza tafsiri kama mchakato wa tafsiri unadhamiriwa kuwa na uamilifu wa zao lenyewe na jukumu hilo hubainishwa na hadhira. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa mikakati iliyotumiwa na watafsiri ilikumbwa na matatizo ya kiisimu na kimtindo yaliyoathiri uelewaji na ufasiri wa ujumbe tafsiri miongoni mwa wasomaji wa vitabu teule. Matatizo hayo yalisabishwa na tafsiri huru, sisisi, mkopo wa moja kwa moja, udondoshaji, unukuzi, uenyeshaji, ugenishaji, na ufidiaji uliofanya matini kuwa aidha finyu au pana. Kwa hivyo, utafiti huu ulichangia na kupanua taaluma ya tafsiri hasa namna ya kuchambua matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini tafsiri za kidini.

APA CITATION

Nyabunga, V. A., Osore, M. & Mwita, L. C. (2023). Tathmini ya Matatizo ya Kiisimu na Kimtindo katika Matini Tafsiri za Kidini: Mfano Wa Njia Salama, Walioteliwa Na Vita Kuu. *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), 55-72. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1639>.

CHICAGO CITATION

Nyabunga, Vince Arasa, Miriam Osore and Leonard Chacha Mwita. 2023. "Tathmini ya Matatizo ya Kiisimu na Kimtindo katika Matini Tafsiri za Kidini: Mfano Wa Njia Salama, Walioteliwa Na Vita Kuu". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (2), 55-72. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1639>.

HARVARD CITATION

Nyabunga, V. A., Osore, M. & Mwita, L. C. (2023) "Tathmini ya Matatizo ya Kiisimu na Kimtindo katika Matini Tafsiri za Kidini: Mfano Wa Njia Salama, Walioteuliwa Na Vita Kuu", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), pp. 55-72. doi: 10.37284/jammk.6.2.1639.

IEEE CITATION

V. A. Nyabunga, M. Osore, & L. C. Mwita "Tathmini ya Matatizo ya Kiisimu na Kimtindo katika Matini Tafsiri za Kidini: Mfano Wa Njia Salama, Walioteuliwa Na Vita Kuu", *EAJSS*, vol. 6, no. 2, pp. 55-72, Dec. 2023.

MLA CITATION

Nyabunga, Vince Arasa, Miriam Osore & Leonard Chacha Mwita. "Tathmini ya Matatizo ya Kiisimu na Kimtindo katika Matini Tafsiri za Kidini: Mfano Wa Njia Salama, Walioteuliwa Na Vita Kuu". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 2, Dec. 2023, pp. 55-72, doi:10.37284/jammk.6.2.1639.

UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Smith (2022), tafsiri ya matini za kidini imekuwa kipengele muhimu katika kueneza ujumbe wa injili katika vipindi vyote vya kihistoria. Vilevile, tafsiri husawazisha mafundisho ya kidini kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Kwa hivyo, makala haya yalitathmini matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini tafsiri za White. Yalichunguzwa ili kuonyesha namna yalivyoathiri uelewaji na ufasiri wa ujumbe tafsiri katika matini teule.

Nida na Taber (1969) wanasema kuwa ni jukumu la mtafsiri kuwakilisha maana asilia katika matini lengwa kwa kuzingatia uwazi na miundo inayokubalika katika lugha inayohusika. Lakini matini teule yalionyesha kuwepo kwa matatizo ya kiisimu na kimtindo yaliyoathiri uelewaji na ufasiri wa ujumbe hali ambayo iliwanyima wasomaji lengwa uwazi na ukubalifu wa vipashio vilivyotafsiriwa. Kwa hivyo, mada hii ilifaa kwa kuwa matini teule zilionyesha kuwepo kwa ukiushi wa uwazi na miundo isiyoeleweka na kufasirika. Kwa hivyo, makala haya yalithminiwa kwa lengo la kuchunguza matatizo ya kiisimu na kimtindo yaliyoathiri uelewaji na ufasiri wa habari katika matini tafsiri.

Vitabu vya White: *Vita Kuu* (1952), *Njia Salama* (1977) na *Walioteuliwa* (2009) ni matini msingi ya kufundishia maadili ya dhehebu la SDA nchini Kenya na maeneo mengine ulimwenguni. Vitabu hivyo vinaendelea kueleweka na kufasirika kwa njia tofauti tofauti miongoni mwa makundi mbalimbali ndani ya dhehebu hilo (Amorim, 1990). Makala haya yalishughulikia lengo kuu la utafiti, matatizo ya kiisimu na kimtindo; misingi

ya kinadharia, mbinu za utafiti, matokeo na uchanganuzi; hitimisho na mapendekezo.

Dhana za Kiisimu na Kimtindo

Kwa mujibu wa Nida (2000), tafsiri ililenga kuwasilisha ujumbe kutoka Lugha asilia (LA) hadi lugha pokezi (LP). Hata hivyo, mara nyingi hukumbana na matatizo ya kiisimu: kisemantiki, kisintaksia na kimofolojia. Naye Newmark (1988) anabainisha aina tatu ya matatizo ya tafsiri: kiurejeshi, kiisimu na kimatumizi. Newmark (ametajwa) afafanua kwamba matatizo ya kiurejeshi husababishwa na namna mambo yalivyo, ulimwengu halisi na umaanisho. Pili, matatizo ya kiisimu yalitokea kwa sababu ya ukosefu wa usarufi, ufahamu wa mitindo ya sentensi, msamiati, na semi za lugha mahususi. Mwisho, matatizo ya kimatumizi hutokea kwa sababu zifuatazo: kutokuwa na uwezo wa kuendeleza maneno kwa usahihi, matumizi mabaya ya kamusi, ukosefu wa visawe na ule wa fahiwa ya kawaida.

Leech na Short (1981) wanafasili mtindo kama taaluma ya kiisimu ambayo lengo lake ni kueleza uhusiano baina ya lugha na majukumu ya kimawasiliano. Hata hivyo, maana ya mtindo inabakia kuwa tata (Boase-Beier, 2006).

Kwa mfano, Snell-Hornby (1995) anasema kuwa mtindo ni daraja inayounganisha vipashio vya kiisimu na kihakiki katika lugha. Kadhalika, daraja hiyo, anawafanya wasomaji kuelewa na kutafsiri matini vyema kupitia uchanganuzi wa kimtindo. Katika makala haya, matatizo ya kimtindo yalikuwa urudiaji wa vipashio vya kisarufi, uradidi, tofauti za kipolisemia na wingi maana za kileksia.

Lengo la Utafiti

Lengo kuu la utafiti lilikuwa tathmini ya matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini teule za White. Tathmini hii ilikuwa muhimu kwa kuwa ililenga kubainisha namna matatizo ya kiisimu na kimtindo yalivyoathiri viwango vya uelewaji na ufasiri wa ujumbe miongoni mwa wasomaji wa SDA.

MISINGI YA KINADHARIA

Makala haya yaliongozwa na nadharia ya skopos. Skopos ilieleza kuwa tafsiri huongozwa na malengo na kuwa si lazima makala asilia (MA) ifanane na makala pokezi (Reiss & Vermeer, 1984). Vilevile, ushirikishi wa mihimili ya nadharia teule ulibainisha kuwa vitabu teule vya White vilikumbwa na matatizo ya kiisimu na kimtindo ambayo yaliosababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe tafsiri miongoni mwa wasomaji lengwa.

Nadharia ya Skopos

Nadharia hii iliasisiwa na Vermeer (1978). Neno *skopos* linatokana na neno la Kigiriki lenye maana “nia ya kutafsiri”. Kwa mujibu wa nadharia hii, kutafsiri ni kuzalisha matini lengwa, kwa kuzingatia lengo, mpokezi na mazingira lengwa (Schaffner, 1998). Nadharia hii ina mihimili mitano, Reiss na Vermeer (1984) katika Munday (2001):

- Uteuzi wa taratibu na mbinu za kutafsiri MP, kunategemea aina ya majukumu ya matini husika.
- Mikdadha ya kiisimu na kitamaduni ya lugha iliyohusika huenda ikafanya majukumu ya MP na MA kuwa tofauti.
- Jukumu la kutafsiri MP katika utamaduni lengwa si lazima lifanane na lile la MA katika utamaduni asilia.
- Matini tafsiri lazima izingatie hali na maarifa ya mpokeaji kwa kuzingatia mshikamano wa ndani wa MP.

- Mtafsiri wa matini tafsiri lazima azingatie viwango vya uaminifu unapohamisha ujumbe kutoka MA hadi MP.

Mihimili ya nadharia hii ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa njia nyingi. Inaweka mkazo kwenye matini lengwa. Nadharia ya skopos inasema kwamba maamuzi yote ya tafsiri yalipaswa kufanywa kuhusiana na lengo la matini pokezi. Hali hiyo ilifanyiwa matini chanzi kimakusudi ili kuleta uaminifu katika mchakato wa kutafsiri (Reiss, 1990).

Matini za kidini hutafsiriwa ili kutimiza malengo fulani ya dini. Ikiwa mtafsiri alilenga kuweka matini kwa lugha halisi iliyoweza kuelewika na msomaji lengwa kwa urahisi bila kupotosha maana, basi alikuwa amefanikiwa katika kutafsiri. Kwa hivyo, nadharia hii ina manufaa katika utafiti kwa kuwa ilisaidia kuchanganua vizuizi vya kiisimu na kitafsiri vilivyosababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe miongoni mwa hadhira lengwa.

MBINU ZA UTAFITI

Dhehebu la SDA nchini Kenya lina miungano miwili ya makongamano: Magharibi mwa Kenya (WKUC) na *East Kenya Union Conference* (EKUC) kwa mujibu wa mipaka ya kiutawala ya SDA (Marundu, 2021). Muungano (WKUC) ulijumuisha kongamano la *Central Nyanza Field, Kenya Lake Conference, Ranen Conference, Western Kenya Conference, North West Kenya Conferences, Nyamira Conference na South Kenya Conference*. Muungano wa EKUC ulijumuisha: *Central Kenya Conferences, Central Rift Valley Conferences na Kenya Coast field*. Kwa mujibu wa utafiti huu, muungano wa WKUC ulishirikishwa pekee, kwa sababu una historia ndefu ya kanisa hilo (Mbwana, 2014). Kwa kuzingatia muungano wa WKUC, miji saba iliteuliwa kimakusudi ili kushirikishwa: Kisumu, Homabay, Ranen, Eldoret, Kitale, Nyamira na Kisii. Katika kila mji kanisa moja wakilishi liliteuliwa. Hoja ya uteuzi wa makanisa hayo ulilenga kupata data wakilishi kwa urahisi. Kadhalika, washiriki walionekana kuwa na sifa na matatizo yaliyofanana. Sampuli ndogo ilikuwa na

faida kubwa kwani vipimo changamano na sahihi vilifanywa kwa tahadhari zote zilizowekwa. Vilevile, hitilafu ya vipimo na upendeleo, ulidhibitiwa kwa urahisi na makosa yalitambuliwa kwa urahisi.

Data ya Utafiti

Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa awamu mbili, kutoka maktabani na nyanjani. Maktabani, vitabu teule (*Vita Kuu, Njia Salama* na *Waliooteuliwa*) vilisomwa kwa kina na matatizo ya kiisimu na kimtindo yalitambuliwa na yalitoa data ya kimsingi ya utafiti huu. Nyanjani, muungano wa WKUC ulishirikishwa. Muungano huo una idadi ya waumini 456501 (Ochorokodi, 2021). Sehemu tu ndogo ya waumini hao ilishirikishwa katika utafiti huu (140), yaani waumini 98 na viongozi 42. Washiriki hao walisailiwa na kuhojiwa kuhusu vipengele vya kiisimu na kimtindo vilivyotatiza uelewaji na ufasiri wa ujumbe tafsiri. Maoni ya washiriki yalikusanywa pamoja na kutoa data sekondari ya utafiti huu.

Kundi Lengwa na Uteuzi wa Sampuli ya Utafiti

Kundi lengwa la utafiti huu lilikuwa wanasabato wa SDA. Kwa hivyo, mtafiti alisoma vitabu teule na kuteua vifungu tatanishi. Vifungu hivyo vilibainishwa. Kwa hivyo, sampuli ya utafiti huu ilikuwa vifungu vilivyo na matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini. Mtafiti alitumia mbinu mbili katika kuteua sampuli ya utafiti huu: Sampuli mtabakishi na sampuli lengwa. Mbinu mtabakishi hurejelea njia ya kugawanya kundi lengwa katika makundi madogo madogo na kisha kuteua kundi wakilishi kutoka kila kundi maalumu (Kombo & Tromp, 2006). Kwa hivyo, vifungu wakilishi vilitathminiwa na kuonyesha namna matatizo ya uelewaji na ufasiri yalivyoathiriwa.

Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa kimaelezo ulizingatiwa na ufafanuzi wa maelezo ya kihesabu kutolewa. Aidha, majedwali na chati yalitumiwa ili kuonyesha mifano mbalimbali ya kiisimu na kimtindo iliyojitokeza katika matini. Data hiyo

ilifasiriwa na kufafanuliwa kwa njia ya mifano na majedwali.

MATOKEO NA MAJADILIANO

Katika sehemu hii, mtafiti aliwasilisha matokeo na majadiliano kwa njia ya maelezo na matumizi ya majedwali. Hali kadhalika, matokeo yaliwasilishwa kwa mujibu wa lengo kuu la utafiti. Mifano na miktadha mbalimbali ilitolewa na kujadiliwa. Kwa hivyo, matokeo yalikuwa matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini teule.

Matatizo ya Kisemantiki

Semantiki hushughulikia vipashio vyote vya kiisimu katika viwango vyote vya lugha. Kuna aina mbili za semantiki: leksia na tungo (Crystal, 1987). Semantiki ya kileksia inachunguza maana za maneno na semantiki tungo inachunguza maana za maneno katika sentensi, kanuni zilizotawala uundaji wa maana ya vishazi na maana ya sentensi nje ya michanganyiko ya utunzi wa leksimu binafsi.

Matatizo ya Kileksia

Leksia ni taaluma inayohusiana na vipashio vya maneno, makundi ya maneno, virai na mofu zao ili kuunda maneno katika lugha. Leksia pia inajishughulisha na aina za maana kama vile: maana dhanishi, maana rejelewa, maana mtindo, maana endanifu, maana shawishi, maana ashirifu, maana ya kisarufi, na maana ya kileksika.

Maana Dhanishi

Harvey na Higgins (2002), wanafafanua maana dhanishi kama vile maana msingi katika kamusi. Maana dhanishi huunda kiunzi cha kuwasiliana kwa kuwa neno husika lina maana msingi moja kwa wasemaji wa lugha moja. Kwa mfano, neno *samawati* lina maana ya *rangi* lakini maana jumlishi ni *huzuni*. Vilevile, tazama namna maneno haya *asali*, *nzi* na *siki* yalivyojitokeza katika mfano ufuatao, kwa kurejelea kitabu cha *Waliooteuliwa*:

Mfano wa 1

MA: *As the old saying goes, you catch more flies with honey than vinegar (The Chosen, uk. 47)*

MP: *Kama usemi wa wahenga usemavyo, unashika nzi wengi kwa kutumia asali kuliko siki (Walioteuliwa, uk 57).*

Nzi ni mdudu mwenye mbawa nne (**TUKI**, 2012) na anapatikana katika mahali pachafu; *asali* ni

maji matamu, mazito ambayo hutengenezwa na nyuki au kutokana na mimea. *Siki* nayo ni maji ya matunda yanayotumiwa kuongezea ladha katika baadhi ya vyakula au dawa. Maneno hayo yote yalipata maana nyingine rejelewa katika muktadha wa matumizi. Kwa hivyo, matokeo yalionyesha kuwa tatizo lenyewe lilikuwa wingi maana wa neno moja katika matini. Tazama *Jedwali la 2:*

Jedwali 1: Maana dhanishi rejelewa

Dhana	Maana dhanishi	Maana rejelewa
Asali	Maji matamu, kutokana na nyuki au mimea	Upendo, uzuri au njia ya kupendeza
Siki	Maji yenye ladha tamu	Upendo au njia ya kutumia maneno matamu
Nzi	Ni mdudu mchafu	Watu walionaswa na dhambi

(**Chanzo:** TUKI, 2012))

Jedwali la 1 lina safu tatu: dhana, maana dhanishi, na maana rejelewa. Kila dhana (*asali*, *siki* na *nzi*) maana dhanishi na rejelewa zilitolewa. Vilevile, dhana hizo ziliibua maana mbalimbali kutegemea miktadha mahususi. Kwa mfano, methali *unashika nzi wengi kwa kutumia asali kuliko kwa kutumia siki* (*Walioteuliwa*, uk 57) ilikuwa na maana mbili: dhanishi na rejelewa. Maana dhanishi ya methali hiyo ilikuwa kwamba, watu wachafu, wabaya waliokwama katika uchafu wa dhambi. Maana rejelewa nayo katika MA ilikuwa, ukitaka kuwarejesha watu wenyemakosa, itakubidi utumie upendo, maneno matamu ili uweze kuwakosoa. Kwa hivyo, uchambuzi huo, ulionyesha kuwa tofauti za maana msingi na maana rejelewa katika MA na MP zilisababisha mianya ya kisemantiki miongoni mwa hadhira lengwa. Katika hali hiyo msomaji alitatizika katika kuelewa na kufasiri maana msingi na maana rejelewa katika matini (Harvey & Higgs, 2002). Ingawa uhamishwaji wa dhana hizo *asali*, *siki* na *nzi* uliwasilisha ujumbe, ulitatiza uelewaji na ufasiri miongoni mwa wasomaji lengwa. Kwa hivyo, matokeo yalidhihirisha kuwa tafsiri haikufanywa kwa kuzingatia majukumu ya washiriki na miktadha ya tafsiri yenyewe (Nord, 2007).

Maana Kimahusiano

Maana kimahusiano hurejelea dhana na sifa zilizohusishwa na neno fulani linapotajwa. Mahusiano ni ule mshiko baina ya neno, kirai, kishazi, au usemi na dhana inayohusishwa na maana ya dhana hizo zinapotajwa au kurejelewa. Matumizi ya maneno ya kimahusiano katika tafsiri yalisababisha utata ikiwa hayajazoeleka miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, neno *Mwa-Adventista* lina maana mahusiano yafuatayo:

- Msabato wa SDA
- Mavazi yake
- Vyakula vyake
- Siku ya Sabato

(**Chanzo :** *Walioteuliwa*)

Katika mfano huo, jina *Mwa-Adventista* lilipotajwa waumini wa SDA walipata maana mahusiano kama ilivyorodheshwa katika mfano (i-iv). Kwa hivyo, matokeo yalionyesha kuwa hali hiyo pia ilieleweka na kufasirika kwa njia tofauti kutoka msabato mmoja hadi mwingine. Wahubiri walipohojiwa kuhusu dhana ya *Mwa-Adventista*, walitoa maoni yafuatayo katika *Jedwali 2:*

Jedwali 2: Utata wa dhana ya MwaAdventista

	Utukiaji	%
Kuzingatia lishe bora	2	28.6
Hali ya maisha imebadilika	2	28.6
Kudumisha mahusiano mema kanisani	1	14.3
Mihimili ya kanisa la SDA	2	28.6
Jumla	7	100.0

(Data ya nyanjani, 2019)

Jedwali la 2 linaonyesha maoni ambayo wahubiri walitoa kuhusu sababu za waumini kutatizika katika kufasiri dhana ya *MwaAdventista*. Majibu yao yalitofautiana kama ifuatavyo: 28.6% walisema kuwa wanasabato wameshindwa kuzingatia lishe bora; 28.6% walisema kuwa hali ya maisha imebadilika; 14.3 % walisema kuwa waumini wameshindwa kudumisha mahusiano mema kanisani na 28.6 % ya waumini walishindwa kufuata mihimili ya kanisa la SDA. Kwa hivyo, ilibainika kuwa maana mahusiano ya dhana ya uadiventista ilitatiza uelewaji na ufasiri wa ujumbe miongoni mwa SDA.

Matatizo ya Haiponimu

Haiponimu ni neno ambalo lina maana mahususi ambayo hujumuishwa katika maana ya neno jingine ambalo lina maana pana (TUKI, 2009). Kwa mujibu wa Lyons (1977), neno *haiponimu* linatokana na maneno mawili ya Kigiriki: *hupo onoma* ambapo *hupo* lina maana ya *kujumuishwa ndani* ya na *onomo* lina maana ya *jina*. Kwa mfano, maneno *mwanamume*, *baba*, *mama*, *mwanamke*, *mtoto*, *mzee*, kila moja lina maana yake mahususi lakini yote huingizwa katika maana ya kijumla ya binadamu. Tafsiri za maneno ya kijumla huwa changamoto katika tafsiri. Tazama leksia za kijumla katika matini ya *Njia Salama*:

Mfano wa 2

MA: *The thorn and the thistle-the difficulties and trials (Steps to Christ, uk. 1)*

MP: *Miti yenye miiba na magugu-yaani shida na majaribu (Njia Salama, uk 1)*

Katika mfano wa 2, maneno haya *thorn* and *thistle* (MA) yana maana mahususi. *Thorn* ni

mwiba na *thistle* ni gugu la Ulaya lenye miiba. Katika MP, maneno hayo mawili yalitafsiriwa kama miti. *Mti* ni mmea wenye shina gumu. Kwa hivyo, maana tafsiri hailingani na ile asilia kwa sababu neno miti ni leksia ya kijumla. Kwa hivyo, ilibainika kuwa kutumia maneno ya kijumla katika matini teule yalisababisha matatizo ya kisemantiki katika tafsiri.

Matatizo ya Kisintaksia

Mifumo ya lugha huwa na mijengeko tofauti ya sentensi kwa sababu kila moja huwa na miundo yake inayokubalika (Ali, 1965). Sintaksia ni kipengele muhimu kinacholazimika kutumiwa katika tafsiri. Mchanganyo wa mifumo ya sentensi ya lugha tafsiri husababisha changamoto za kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Baadhi ya matatizo ya kisintaksia yanayojitokeza katika tafsiri mara nyingi huwa ya njeo, mpangilio wa maneno na utata wa kupanga sentensi katika matini.

Matatizo Yaliyotokana na Uteuzi mbaya wa Viambajengo katika Sentensi

Viambajengo vya sentensi vinajumuisha neno, kirai na kishazi (Massamba, 2004). Yang (2010) anasema kuwa uteuzi wa maneno, virai na vishazi wa vipashio usio sahihi husababisha matatizo ya kisintaksia katika tafsiri. Tazama mfano:

Mfano wa 3

MA: *Choosing sides in the war of all wars.*

MP: *Kuchagua upande katika vita ya vita zote (Chanzo: Walioteuliwa)*

Mfano wa 3, kirai *choosing sides* kilitafsiriwa kama *kuchagua upande*. Kwa hivyo, kirai tafsiri kilizalisha maana tofauti katika MP. Kwa mfano,

neni *sides* katika MA lina dhana ya wingi lakini tafsiri yake ilikuwa ya umoja. Kwa hivyo, tofauti hiyo ilisababisha matatizo ya kisintaksia katika makala pokezi mtafsiri alimnyima msomaji nafasi ya kuchagua upande alikotaka lakini katika MA, mwandishi alitoa nafasi zaidi ya moja ya kuchagua katika mapambano ya vita. Vilevile, kirai *war of all wars* kilitafsiriwa kama *Vita ya vita zote*. Katika tafsiri hiyo, mtafsiri alihamisha ujumbe kwa kuzingatia muundo wa LA. Kwa hivyo, matokeo yalionyesha kuwa miundo ya lugha ilitofautiana. Tafsiri ya *war of all wars* ni tofauti na *vita ya vita zote* kwa kuwa Makala asilia ilileta dhana ya wingi ilhali Makala pokezi ilileta dhana ya umoja. Hali kadhalika, anwani *Choosing sides in the war of all wars* ilikuwa dhana ya wingi (MA) lakini ilihamishwa kama dhana ya umoja na kwa hivyo kuwanyima wasomaji wa MP usahihi na usawa wa ujumbe. Mwongozo wa *skopos* unatoa hoja kwamba, mtafsiri lazima awe mwaminifu anapohamisha ujumbe wake (Reiss & Vermeer, 1984). Tazama mfano:

Jedwali 3: Uteuzi mbaya wa viambajengo

MA	MP	Tafsiri yetu
Consider this great challenge	Tafakari changamoto <i>moto hii kuu</i> (uk 6)	Tathmini changamoto hii kuu
... and they would have the testimony of Jesus, which is the Spirit of Prophecy.	... na watakuwa na ushuhuda wa Yesu, <i>ambayo</i> ni Roho ya unabii (uk 7)	... na watakuwa na ushuhuda wa Yesu, ambao ni ya roho ya unabii
It's the story of the long contest between good and evil that began thousands of years ago and is not yet finished.	Ni kisa cha pambano la muda mrefu baina ya wema na uovu <i>lilianza</i> miaka maelfu iliyopita na bado haijaisha	Ni kisa cha pambano cha muda mrefu baina ya wema na uovu kilichoanza miaka maelfu iliyopita na bado kinaendelea.
An unbroken line of loyal	Mfululizo wa waaminifu usiokatika	Ukoo wa waaminifu usiokatika
Winning the rebels through love	Kuwarejesha waasi kwa njia ya upendo	Kuwasawishi waasi kwa upendo
Looking for the wrong King	Kukosea katika kumtazamia Mfalme	Kumtafuta mfalme asiyewajibika
The saving life and death of Jesus provided free salvation for everyone. (Pg 52)	Maisha ya kuokolewa kupitia kifo cha Yesu vimeleta wokovu wa bure kwa kila mtu. (uk 63)	Kuokolewa kwa maisha na kifo cha Yesu vimetoa uhuru wa uokovu kwa kila mmoja.

(Chanzo: *Walioteuliwa*)

Jedwali 3 lina mifano saba iliyoonyesha matatizo ya kisintaksia yaliyotokana na uteuzi mbaya wa maneno, virai na vishazi katika sentensi. Mathalan, kishazi *consider this great challenge*

Mfano wa 4

MA: *The Called ... The Chosen*, written by Ken McFarland, originates with the “big picture” vision of Hollis Scarbrough and confirms the following statement:

MP: Kitabu hiki cha *Wateule* kimeandikwa na Ken McFarland kutoka kwenye *njozi ya Mtazamo mkuu wa Hollis Scarbrough ambayo inathibisha na kauli ifuatayo* (uk 5).

Katika mfano wa 4, kirai “big picture” kilitafsiriwa kama *njozi ya mtazamo mkuu* wa Hollis Scarbrough. Dhana ya *njozi ya mtazamo mkuu* ilikuwa tofauti na *maono ya mtazamo mkuu*. Kwa sababu *njozi* na *maono* ni leksia tofauti. Tafsiri ya aina hiyo ilisababisha matatizo ya kisintaksia.

Jedwali 3 lifuatalo lilionyesha tafsiri zenye matatizo yaliyotokana na uteuzi wa maneno mbaya wa viambajengo katika sentensi:

kilitafsiriwa kama *tafakari changamoto moto hii kuu* (*Walioteuliwa*, uk. 6). Mwandishi katika MA alilenga kutathmini changamoto iliyopo ili afanye maamuzi. Lakini katika MP ilileta dhana ya

kufikiria bila kumpa msomaji nafasi afanye maamuzi. Vilevile, neno *Consider* lilileta dhana ya kuwepo na urejeleshi zaidi ya mmoja katika matini ilhali *tafakari* haina urejeleo wote. *Tafakari* kwa mujibu wa kamusi ya Webster (1828) ni upataji wa wazo katika akili; si lazima ulichunguze na kulifanyia maamuzi. Hali hiyo iliufanya ujumbe katika matini hizo mbili kutolingana kimaana. Kwa hivyo, tafsiri ya kishazi *consider this great challenge* ilisababisha matatizo ya kisintaksia.

Anwani ya pili nayo iliamishwa kwa kuzingatia usawa wa ujumbe katika makala zote mbili; ila tu tatizo la kisarufi lililojitokeza katika MP pale ambapo kirejeshi *which* ambacho kilirejelea ushuhuda kilitafsiriwa kama *ambayo*. Kirejeshi hicho hakina upatanisho wa ngeli. Kwa hivyo, tafsiri ya *...and they would have the testimony of Jesus, which is the Spirit of Prophecy* ingekuwa *... na watakuwa na ushuhuda wa Yesu wenye roho ya unabii*. (TY).

Anwani ya tatu (Jedwali la 3), mtafsiri aliamisha sentensi *It's the story of the long contest between good and evil that began thousands of years ago and is not yet finished* kama ni kisa cha pambano la muda mrefu baina ya wema na uovu lilianza miaka maelfu iliyopita na bado haijaisha. Katika MA vipatanishi vya ngeli vilizingatiwa lakini katika MP, havikuzingatiwa. Kwa mfano, kishazi *that began thousands of years ago and it is not yet finished* hakilingani kimaana na lilianza miaka maelfu iliyopita na bado haijaisha. Kirai and it is not yet finished kilirejelea pambano ambalo bado linaendelea. Kitenzi haijaisha katika MP hakibainishi kitu ambacho hakijaisha. Dhana ya kishazi bado haijaisha hairejelei pambano kama ilivyojidhihirika katika MA bali ilirejelea miaka badala ya pambano. Kwa hivyo, tafsiri hiyo iliwanyima wasomaji usawa wa kimaana.

Anwani ya nne, Jedwali la 3, *An unbroken line of loyal* ilitafsiriwa kama *mfufulizo wa waaminifu usiokatika*. Kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya kauli hiyo, ujumbe huo ulirejelea kundi la watu ambao walikuwa waaminifu katika vipindi mbalimbali vya uenezi wa injili. Dhana ya *line of loyal* ilidondoshwa katika MP; pia dhana

hiyo ilitafsiriwa kama *mfufulizo*. Tafsiri ya *An unbroken line of loyal* ingekuwa *ukoo wa waaminifu usiokoma* (TY). Matokeo yalionyesha kuwa uzingatiaji wa miktadha ya kiisimu ilikuwa suala la kimsingi katika tafsiri kama mwongozo wa nadharia ya tafsiri-tendo unavyoeleza (Holz-Manttari, 1984).

Anwani ya tano katika (Jedwali la 3) *Winning the rebels through love* ilitafsiriwa kama *kuwarejesha waasi kwani njia ya upendo*. Dhana ya *winning the rebels* katika MP, ilitafsiriwa kama *kurejesha waasi*. *Winning* katika MA ililenga dhana ya kuwashawishi walioasi maadili warudi kanisani. Lakini katika MP, neno la kijumla *kuwarejesha* lilitumiwa. Neno hilo halileti dhana asilia kwa njia ya kimuktadha. Kwa hivyo, uhamishwaji huo ulikuwa na upungufu kwa mujibu wa nadharia ya skopos inayotoa mwongozo kuwa mtafsiri angefaa kuzingatia miktadha ya kiisimu ili kuleta usawa wa kimaana (Reiss & Vermeer, 1984).

Anwani *looking for the king* imetafsiriwa kama *kukosea katika kumtazamia mfalme* (mfano wa 6 katika (Jedwali la 3). Mwandishi alisema kuwa watu walishindwa katika kumtafuta mfalme aliyewajibika. Katika uhamishwaji huo maana msingi haikujitokeza kwa sababu ya uteuzi mbaya wa viambajengo kama vile virai *looking for* na *wrong King* ambavyo havikuhamishwa hadi MP.

Matatizo yaliyotokana na Udondoshaji na Uongezaji wa Vipashio

Katika matini teule kuna baadhi ya maneno, virai, vishazi ama sentensi zilizodondoshwa au kuogezwa katika makala tafsiri. Udondoshaji huo ulisababisha matatizo ya kisintaksia na hatimaye kuuathiri ujumbe uliotarajiwa uwafikie walengwa kama ilivyodhihirika katika mfano ufuatao:

Mfano wa 5

MA: *Nature and revelation alike testify of God's love. Our Father in heaven is the Source of life, of wisdom, and of joy.*

MP: *Viumbe vya ulimwengu na jinsi Mungu alivyowafunulia wanadamu mambo yajayo,*

vyote huonyesha upendo wake Mungu (Njia Salama)

Mfano wa 5 ulionyesha matatizo yaliyotokana na udondoshwaji wa kimaana. Kwa mfano, kishazi *nature and revelation* kilitafsiriwa kama *Viumbe vya ulimwengu*. Katika tafsiri hiyo neno la kimsingi *ufunuo* (revelation) lilidondolewa na kutupiliwa mbali. Vilevile, vipengele kama vile *mambo yajayo*, *vyote huonyesha* viliongezewa katika MP. Basi, ujumbe wa *ufunuo* haukuhamishwa hadi makala pokezi. Kwa mujibu ya nadharia ya tafsiri-tendo, tafsiri ni uzalishaji wa makala yenye uamilifu wa kimawasiliano kwa msomaji (Holz-manttari, 1984). Vilevile, ujumbe katika MA uliwasilishwa kwa sentensi huru mbili lakini katika MP sentensi hizo zilidondoshwa. Kwa hivyo, matokeo yalionyesha kuwa udondoshi huo uliondoa dhana muhimu katika MT kama vile *ufunuo*, *ushuhuda*, *hekima* na *furaha ambazo zilikuwa sehemu ya maana msingi katika MA*. Tazama mfano:

Mfano wa 6

MA: *He is slow to anger and of great kindness.*

MP: *Si mwepesi wa hasira (Njia Salama, uk 2)*

Katika mfano wa 1.6, dhana ya uambatani ilidondoshwa. Sentensi *He is slow to anger and of great kindness* iliundwa na sentensi sahili mbili zilizojisimamia kimaana. Lakini mtafsiri aliihamisha sentensi hiyo kwa njia tofauti kwani kirai cha *and of great kindness* kilidondoshwa katika MP. Ujumbe asilia *slow to anger* na *great kindness* haukuhamishwa kwa uaminifu. Kwa hivyo, ujumbe si *mwepesi wa hasira na mwingi wa rehema* uliondolewa katika MP. Kwa hivyo, mtafsiri aliwanyima wasomaji sehemu muhimu ya maana. Tazama mfano:

Mfano wa 7

MA: *The lord hath anointed me to preach the gospel to the poor*

MP: *Kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiria masikini habari njema (Njia Salama, uk 62).*

Katika mfano wa 7, sentensi *the lord hath anointed me to preach the gospel to the poor* ilitafsiriwa kama *kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiria masikini habari njema*. Katika tafsiri hiyo kirai *The Lord* kilidondoshwa katika MP na kwa hivyo, kufanya sentensi hiyo kukosa mtendaji. Tafsiri hiyo ingekuwa *Bwana ametia mafuta ili niwahubirie masikini injili*. Katika MP aliyemtia mafuta hakubainishwa kama ilivyo katika MA. Hali hiyo ilikuwa changamoto kwa hadhira lengwa na msomaji aliyesoma makala zote mbili alihisi kwamba makala pokezi ilikuwa tofauti ikilinganishwa na makala asilia. Kwa hivyo, utathmini huo ulionyesha kuwa matatizo ya udondoshaji katika matini teule yalisababisha ukosefu wa ushikamano na muumano wa ujumbe kama nadharia ya skopos inavyodokeza (Reiss & Vermeer, 1984).

Matatizo yaliyotokana na Tafsiri za Virai na Vishazi

Tafsiri za maneno, virai, vishazi, na sentensi ilibabisha matatizo ya kisintaksia. Matatizo hayo yalisababishwa wakati vipashio vilipokuwa vinahamishwa kutoka lugha moja hadi ya nyingine Kuhusu matatizo ya virai na vishazi, Mathieu (2003) anaeleza kuwa tofauti za vipashio vya kisarufi baina ya lugha mbili zinazohusika husababisha matatizo ya kitafsiri. Tazama mfano ufuatao:

Mfano wa 8

MA: *When Jesus revealed to his disciples the fate of Jerusalem and the scenes of the second advent, he foretold also the experience of his people from the time when he should be taken from them.*

MP: *Yesu alipowafunulia wanafunzi wake ajali itakayoujia mji wa Yesulemu na Mambo yatakayooekana katika marejeo yake, aliwaambia pia juu ya hali ya maisha ya watu wake tangu atakapochukuliwa (Vita Kuu, uk 49)*

Data ya mfano wa 8, kirai *the fate of Jerusalem* kilitafsiriwa kama *ajali itakayoujia Yesulamu*. Katika kirai hicho, maana ya neno *fate* ilikuwa si sawa na neno *ajali kama ilivyotafsiriwa*. Katika muktadha wa MA, mwandishi alikushuhudia kueleza hatima ingeliupata mji wa Yerusalemu na wala si ajali kama ilivyoenezwa. Hali hiyo ilifanya MP kuwa tofauti na kwa hivyo, kwenda kinyume na nadharia ya utafiti huu iliyotoa mwongozo kuwa mtafsiri lazima azingatie viwango vya uaminifu katika tafsiri.

Vilevile, kishazi *he foretold* kilitafsiriwa kama *aliwaambia*. Lengo la MA lilikuwa kutabiri lakini katika MP lilibadilika na kuwa kufahamisha. Kutabiri na kufahamisha ni dhana mbili tofauti. Kutabiri ni kusema kuwa kuna tukio litakalotokea siku zijazo na kufahamisha ni kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kinywa au maandishi. Hali hiyo pia ilifanya ujumbe tafsiri kuwa tofauti. Tazama mfano mwingine:

Mfano wa 9

MA: *Little by little, at first, he stealth and silent, and then more openly as it increased in strength and general control of the minds of men, the mystery of iniquity carried forward its deceptive and blasphemous work.*

MP: *Pole pole kwa hila na kwa siri mwanzoni, ile siri ya kuasi iliendeleza kazi yake ya udanganyifu na kumtukana Mungu; lakini kwa kadri ilivyozidisha nguvu na kuzitawala nia za watu, hivyo ndivyo alivyozidi kufanya kazi yake kwa wazi (Vita Kuu, uk 49)*

Katika mfano wa 9, mtafsiri alitafsiri habari kwa njia ya kisemantiki bila kuzingatia tofauti za miundo na utaratibu wa lugha pokezi. Kwa mfano, kishazi *Little by little, at first in stealth and silent* kilitafsiriwa kama *Pole pole kwa hila na kwa siri mwanzoni*. Kirai *little by little* kisawe chake si *pole pole* kama ilivyotafsiriwa. Muktadha wa matumizi ya kirai hicho (MA) ulileta dhana ya vipimo au viwango; na ule wa MP ulileta dhana ya kasi ambayo si ya haraka. Kwa hivyo, tafsiri ya

virai na vishazi hivyo ulisababishwa na matatizo ya kiisimu.

Vilevile, maana ya kifungu and then more openly as it increased in strength and general control of the minds of men, kiliamishwa kama lakini kwa kadri ilivyozidisha nguvu na kuzitawala nia za watu, hivyo ndivyo alivyozidi kufanya kazi yake kwa wazi. Matumizi ya kiunganishi **and** katika MA yalileta dhana ya kiunganisha. Kisawe tafsiri cha and kilikuwa **na**. Na katika muktadha huo kilikuwa kiambishi ambatanishi kilichotumiwa kiunganisha vishazi viwili au zaidi ambavyo vililingana kimaana. Kwa hivyo, kutafsiri and kama lakini kulipotosha wasomaji. Kiunganishi **lakini** kisawe chake ni **but** katika Kiingereza. Lakini ni kiunganisha ambatanishi kinachotumiwa kutoa habari tofauti na ile tayari ilikwishatajwa. Sentensi hii the mystery of iniquity carried forward its deceptive and blasphemous work ilitoka katika kishazi cha pili na kwa hiyo kilifaa kuambatanishwa na kiunganishi kamili **na** wala si **lakini**. Tafsiri hiyo ingekuwa na tena kadri alivyozidisha uwezo na mamlaka yake kwa jumla; aliteka akili za watu (TY). Kwa ufupi, ujumbe katika sentensi hiyo ulivurugika kiasi cha sentensi kuonekana tofauti. Tafsiri ya aina hiyo ilisababisha matatizo ya kiisimu miongoni mwa wasomaji lengwa. Uchambuzi huo ulionyesha kuwa matatizo hayo yalitokana na mtafsiri kushindwa kuzingatia muktadha ya kiisimu ya lugha mbili husika katika kutafsiri virai na vishazi katika tungo.

Katika matini teule, mtafsiri alivuruga masuala mengi ya kisintaksia kama inavyojidhihirisha katika mifano iliyopo hapo juu. Ingawa alilenga mahitaji ya wasomaji wasioelewa Kiswahili kwa ufasaha, aliamishwa ujumbe mbalimbali kwa njia tatanishi. Ukiushi huo unarandana na matakwa ya nadharia ya skopos kuwa matini chanzi si lazima ifanane na matini pokezi, kwani tafsiri inaongozwa na malengo (Reiss & Vermeer, 1984). Hata hivyo, matokeo yalionyesha kuwa tafsiri hiyo ilikiuka miundo na mipangilio ya virai, vishazi na sentensi katika sintaksia ya Kiswahili.

Matatizo ya Kimofolojia

Mofolojia ni tawi la isimu ambalo huchunguza maumbo ya maneno na aina zake. Tawi hili la isimu hushughulikia hasa kipashio cha neno (Mathew, 1974; Hartman, 1972, na TUKI 1990). Katika lugha yoyote ile, vipashio vya kimofolojia ndivyo huunganishwa ili kuzalisha vipashio vikubwa zaidi ambavyo vinakuwa ama neno, kirai, kishazi na sentensi. Ujenzi huu wa vipashio hutegemea mfumo wa lugha inayohusika. Kando na hayo, mtafsiri hulazimika kupanga vipashio

hivyo vya kimofolojia kwa njia iliyokubalika katika lugha ndipo maana za vifungu vya maneno ipatikane na kueleweka kwa hadhira lengwa.

Matatizo yaliyotokana na Makosa ya Maendelezo

Maneno ambayo hayapatikani katika kamusi yalirejelewa kama makosa ya tahajia au maendelezo. Haya yakuwa makosa ya uchapaji yaliyofanywa katika matini tafsiri. Data ya utafiti huu ilibaini kuwa kuna matatizo ya kimofolojia katika matini tafsiri. Tazama *Jedwali 4* lifuatalo:

Jedwali 4: Makosa ya Maendelezo

Kitabu	MA	MP	Sahihi
Njia Salama	Grace	Noema	Neema
	Atone	Kudhibiwa	Kuadhibiwa
	That	Hate	Hata
	Others	Wengino	Wengine
	Except be born again	Asapozaliwa	Asipozaliwa
	From	Tangi	Tangu
	We shall not renounce	Katuwozi	Hatuwezi
	Bring upon	Mbole	Mbele
	No genuine repentance	Hakugouka	Hakugeuka
	Grace	Neeraa	Neema
	Slow to anger	Si mpesi	Si mwepesi
	To preach	Kuwahubiri	Kuwahubiria

(Chanzo: Njia Salama)

Jedwali la 4 lina safu zifuatazo: Matini teule, makala asilia, makala pokezi na maendelezo sahihi. Data hiyo ilionyesha neno asilia, tafsiri yake na maendeleo sahihi ya neno lenyewe. Kwa mfano, maneno yafuatayo yaliamishwa na kuendelezwa kimakosa: *grace* kama *noema*, *that* kama *hate*; *from* kama *tangi* na *slow to anger* kama *si mpesi*. Tahajia za maneno hayo: *noema* (neema), *hate* (hata), *tangi* (tangu), *mbole* (mbele) na *neera* (neema) zilitatizo usomekaji wa ujumbe. Makosa ya tahajia yalikuwa mzigo kwa upande wa hadhira kwa sababu ya kutatizika kupata maana lengwa. Tahajia mbaya pia ilileta mkanganyiko, kupoteza uwazi na maana ya matini tafsiri.

Munday (2016) anasema kuwa kanuni ya ushikamano ni muhimu katika tafsiri kwa sababu inaweka mkazo kwenye muumano wa kimatini. Hiyo ilimaanisha kuwa tafsiri lazima ikubalike, iwe na maana kwa kuzingatia viwango vya uaminifu.

Matatizo yaliyotokana na Uunganishwaji na Utenganishwaji wa Maneno

Matatizo ya uunganishwaji katika matini ya *Walioteuliwa* yalikuwa pamoja na uunganishwaji wa maneno, utenganishwaji na maendeleo yasiyo sahihi. Tazama *Jedwali 5* lifuatalo:

Jedwali 5: Matatizo ya uunganishwaji wa maneno

Kitabu	MA	MP	Sahihi
<i>Walioteuliwa</i>	Are you sure To see themselves superior To find out And every Because Dark	Unauhakika Nakujidhania Ilikugundua Nakila Kwasababu Utusiutusi	Una uhakika Na kujidhania Ili kugundua Na kila Kwa sababu Utusi tusi

(Chanzo: *Walioteuliwa*)

Jedwali 5 lina data ya makosa ya uunganishwaji wa maneno. Kwa mfano, maneno yafuatayo yameunganishwa: *unauhakika* (Una uhakika); *nakujidhania* (na kujidhania); *ilikugundua* (ili kugundua); *nakila* (na kila); *kwasababu* (kwa sababu) na *utusutusi* (utusi tusi). Maneno mawili yakiunganishwa pamoja yanaleta dhana tofauti za kisemantiki katika tafsiri kama inavyojitokeza katika *Jedwali hili*. Kwa kuzingatia mwongozo

wa nadharia kuwa mtafsiri wa matini tafsiri lazima azingatie viwango vya uaminifu anapohamisha ujumbe kutoka MA hadi MP. Kwa hivyo, uunganishwaji wa namna hiyo ulisababisha matatizo ya kiisimu katika matini ya *Walioteuliwa*. Hali kadhalika, kulikuwa na makosa ya utenganishwaji wa maneno mawili katika matini hiyo. Tazama *Jedwali la 6*:

Jedwali 6: Utenganishwaji wa Maneno

Kitabu	MA	MP	Sahihi
<i>Walioteuliwa</i>	One of On the air When seen When you hear Accepted Evicted Invades Eradicates Apart	Mmoja wapo Ulipo rushwa Ulipo onekana Ukisha sikia Yana kubalika Walivyo fukuzwa Yanapo vama Atakapo ondoa Mbali mbali	mmojawapo uliporushwa ulipoonekana ukishasikia Yanakubalika Walivyofukuzwa Yanapovamia Atakapoondoa Mbalimbali

Chanzo: *Walioteuliwa*

Jedwali la 6, lilidhihirisha makosa yaliyotokana na utenganishwaji wa maneno. Kwa mfano, maneno: *one of* (mmoja wapo); *on air* (ulipo rushwa); *when seen* (ulipo onekana); *when you hear* (ukisha sikia); *accepted* (yana kubalika); *evicted* (walivyo fukuzwa); *invades* (yanapo vama); *eradicates* (atakapo ondoa) na *apart* (mbalimbali) yalitenganishwa. Kwa hivyo, matatizo hayo yalisababisha matatizo ya kisarufi.

Matatizo yaliyotokana na Uundwaji wa Maneno

Uundaji wa istilahi za Kiswahili ambao umekuwa ukiendelea tangu mwaka 1930 umekuwa ukikabiliwa na matatizo yaliyotokana uundaji wa maneno yenye makosa ya kisarufi. Matatizo hayo, yalijumuisha upungufu mkubwa wa istilahi

takribani nyanja zote za taaluma (Mwansoko na wengine: 1992). Dhana za kisarufi huundwa kwa njia isiyofuata muundo wa lugha lengwa. Tazama mfano:

Mfano wa 10

MA: *Satan's deceptions*

MP: *Madanganyifu ya Shetani* (Chanzo: *Walioteuliwa*)

Mfano wa 10, kirai *Satan's deceptions* kilitafsiriwa kama *madanganyifu ya Shetani*. Katika tafsiri hiyo, vitendo vya udanganyifu vilimilikiwa na shetani. Kwa kuwa vitendo hivyo vilikuwa vingi, mtafsiri alivitaafsiri kama madanganyifu na kusababisha tatizo la kisarufi kwa sababu nomino dhahania ya udanganyifu

haina wingi kimaandishi. Mofu kapa ya wingi ilikuwa dhahania na kwa hivyo, haingeweza kudhihirika kimaandishi. Kwa kutozingatia muundo wa lugha pokezi, tafsiri hiyo ilikiuka mwongozo wa nadharia ya tafsiri-tendo, kuwa tafsiri ni mchakato wa kupitisha ujumbe kati ya lugha chanzi na pokezi kwa viwango vilivyo sawa (Nord, 2007).

Matatizo ya Kimtindo

Kwa mujibu wa TUKI (2012) mtindo ni namna ya kutafsiri. Ni matokeo ya mtafsiri kuteua baadhi ya miundo katika lugha. Mchakato huo ni pamoja na uteuzi wa maneno na miundo ya sentensi katika tafsiri. Leech na Short (1981) wanafasili mtindo kama taaluma ya kiisimu ambayo lengo lake ni kueleza uhusiano baina ya lugha na majukumu ya kimawasiliano. Kwa hiyo, msomaji akiwa hana uzoefu wa kimatini, kimtindo na kiutanzu hataweza kuelewa matini anayaoisoma. Tazama mfano *Njia Salama*:

Mfano wa 11

MA: *“The eyes of all wait upon Thee;*

And Thou givest them their meat in due season.

Thou openest Thine hand,

And satisfiest the desire of every living thing.” (Psalms 145:15, 16).

MP: *“Macho yao wote yakutazamia wewe;*

Nawe huwapa chakula chao majira yake.

Hufunua mkono wako,

Humshibisha kila hai uradhi.” (Zaburi 145:15,16).

Shairi la 11 liliwasilishwa kwa mitindo miwili tofauti, kirasimi na kisasa. Mtindo wa kirasimi ulitumia *Thee, Thou, Thine, givest, openest na satisfiest*. Maneno hayo yalikuwa na matumizi maalum. Kwa mfano, *Thee, Thou na Thine* yalipotumiwa katika matini ya kidini yalimrejelea Mungu. Kwa hivyo, kutafsiri maneno hayo na

kuhifadhi mitindo yenyewe katika lugha pokezi ilikuwa changamoto. Kwa mfano, kishazi *the eyes of all wait upon Thee* kilitafsiriwa kama *Macho yao wote yakutazamia wewe*. Katika MA matumizi ya *Thee, Thou na Thine*, yalibainisha wazi kuwa aliyehusika ni Mungu lakini katika MP, maneno *wewe, yake na wako*, hayakubainisha wazi aliyehusika kwa njia ya wazi. Vilevile, matumizi ya maneno *givest, openest na satisfiest* yalibainisha wazi kuwa Mungu ndiye huwapa, hufunua na kuwatosheleza watu. Tofauti za mitindo tofauti hiyo iliwanyima wasomaji ladha asilia ya MA. Tazama mfano mwingine wa ushairi:

Mfano wa 12

MA: *The Lord “hath anointed Me to preach the gospel to the poor;*

He hath sent Me to heal the brokenhearted,

to preach deliverance to the captives,

and recovering of sight to the blind,

to set at liberty them that are bruised.” (Luke 4:18, uk 11)

MP: *“Roho ya Bwana ni juu yangu,*

Kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema.

Amenituma kuwaponya waliopondeka moyo,

Kuwatangazia wafungwa kufunguliwa,

na vipofu kupata kuona tena,

Kuwaacha wa huru waliosetwa.” (Luka 4:18. Uk 3)

(**Chanzo** : *Njia Salama*)

Katika mfano wa 12 mtafsiri alitumia mtindo wa kimaalezo ilhali wa MP ulikuwa wa kishairi. Kwa hivyo, uhamishaji wa aina hiyo ulikanganya wasomaji wa matini lengwa. Kwa mfano, sentensi *The Lord “hath anointed Me to preach the gospel to the poor* iliamishwa kwa mishororo miwili iliyo tofauti kama inavyojidhihisha hapa chini:

“Roho ya Bwana ni juu yangu,

Kwa sababu amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema.

Ingawa mtafsiri alipitisha ujumbe kwa hadhira, uliwasilishwa kwa mtindo tofauti pasi kuzingatia usahihi wa ujumbe na kwa hiyo kutatiza wasomaji wa makala pokezi kwani ulionekana kuwa tofauti. Tofauti za mitindo ya uzungumzaji baina ya LC na LL, ni tatizo katika tafsiri. Hali hiyo ilijitokeza kwa sababu mtindo mmoja uliweza kutumika katika muktadha fulani lakini ukashindwa kupata tafsiri kwa lugha nyingine katika muktadha ule ule.

Matatizo yaliyotokana na Urudiaji

Urudiaji katika matini teule ulijitokeza katika viwango vya neno, kirai, kishazi na sentensi. Kutafsiri neno au mafungu ya maneno yaliyorudiwa katika MA hadi MP ilikuwa hali ambayo iliathiri maana msingi. Kwa sababu ukiondoa kipashio kilichorudiwa katika matini asilia, nia asilia mwandishi ilipotea. Tazama mfano:

Mfano wa 13 (Walioiteuliwa)

MA: *With the flood, the line of faithful had been given a chance to survive –and survive, it did.*

MP: *Kutokana na gharika, ukoo mwaminifu umepewa nafasi mpya ya kuishi-na kuendelea kuishi.*

Katika mfano wa 13, dhana ya urudiaji ilijitokeza. Kwa mfano, maneno *survive- and survive, it did* yalirudiwa. Marudio hayo yalitafsiriwa kama *kuishi-na kuendelea kuishi*. Dhana ya *survive-and survive, it did* ilileta maana ya kudumu na kudumu. Lakini katika MP, dhana hiyo ilibadilika na kuwa *kuishi* na *kuishi*. Kudumu na kuishi ni dhana mbili tofauti. Hali hiyo ilzalisha tafsiri pana au kuongeza vipashio ambavyo havikuwepo katika MA. Kwa mfano, sentensi *the line of faithfuls had been given a chance to survive* ilitafsiriwa kama *ukoo mwaminifu umepewa*

nafasi mpya ya kuishi. Katika tafsiri hiyo vipashio *ukoo na mpya* havikuwepo katika makala chanzi.

Vilevile, tafsiri ya *the line of faithfuls* ingekuwa *kundi la waaminifu*. Uhamishwaji wa ujumbe wa aina hiyo ulisababisha utata uliotokana na tofauti za kimtindo. Mwongozo wa nadharia ya skopos ulitoa kauli kuwa lazima mtafsiri azingatie miktadha ya kiisimu anapotafsiri matini ili kudumisha muumano wa unaofanana na MA (Nord, 2007).

Kwa mujibu wa Ghazala (2008), uradidi ni matumizi ya maneno ya ziada yasiyo ya lazima katika kauli ili kueleza jambo fulani. Maelezo ya Ghazala yalizingatiwa kutathmini matatizo yaliyotokana na uradidi katika matini teule. Kwa mfano, *peta-petapeta; pika-pikapika; Waadventista Wasabato na Walioitwa - Walioiteuliwa*. Maneno hayo yalirejelea dhana ile ile na kwa hiyo hayakuwa na maana ya kuyarudia kwa sababu dhana hiyo ilieleweka. Hata hivyo, kutafsiri semi na dhana za aina hiyo kulisababisha matatizo ya kitafsiri. Tazama *mfano*:

Mfano wa 14

(a) **MA:** *They love pleasure and self-indulgence* (Uk. 19)

MP: *“Wao pia hupendezwa na anasa ya kidunia kama nipendezewayo mimi.”*

(b) **MA:** *Here is where thousands upon thousands have erred to their eternal loss.*

MP: *Watu wengi hukosa katika jambo hilo (Njia Salama, uk 19).*

c) **MA:** *Every act of transgression, every neglect or rejection of grace of Christ...* (uk. 20).

MP: *Kila tendo baya, kila mara unapoidharau na kuitupia mbali neema ya Kristo,*

Katika mfano wa 14 (a) dhana ya uradidi ilijitokeza. Kwa mfano, dhana ya *pleasure* (anasa) nayo *self-indulgence* (kubugia) katika *anasa*. Ingawa uradidi huo uliweka mkazo kwenye kile

kilichoelezwa, ulisababisha matatizo katika kitafsiri. Kwa mfano, kishazi *they love pleasure* kilitafsiriwa kama *wao pia hupendezwa na anasa*. Katika uhamishwaji huo, kulitokea uradidi usio wa lazima kwani ulifanya tafsiri kuwa legevu. Kwa hivyo, maelezo hayo yalionyesha kuwa uradidi katika tafsiri husababisha matatizo ya kimtindo.

Pili. mfano wa 14(b) ulionyesha uradidi. Kwa mfano, neno *thousands* lilirudiwa katika *thousands upon thousands*. Uradidi huo ulikuwa muhimu kwa sababu ulifanya ujumbe asilia kueleweka kwa wazi lakini ujumbe huo ulipotafsiriwa ulizua matatizo ya kitafsiri. Kwa mfano, kishazi *Here is where thousands upon thousands have erred to*

their eternal loss kilitafsiriwa kama *Watu wengi hukosa katika jambo hilo*. Uhamisho huo ulionyesha kuwa zao lilikua tofauti. Uradidi wa MA haukuhamishwa na kwa hivyo, matatizo ya kisarufi yaliyotokana na tofauti za miundo.

Matatizo yaliyotokana na Tofauti za Polisemia

Dhana ya polisemia imeelezwa na wataalamu mbalimbali (Crystal, 1991). Crystal anaeleza kuwa polisemia ni faridi ya kileksia ambayo ina maana tofauti tofauti. Kwa mfano, neno **wazi** lina maana anuwai: **kiwango, kisichopambwa, kisichozuliwa, dhahiri, kinachoonekana na cha kawaida** (Merriam-Webster, 2008. Tazama Jedwali la 7:

Jedwali 7: Mifano ya Polisemia

Kiingereza (LA)	Kiswahili (LP)
Man	Binadamu, kiume,
Bright of decay	Mianga ya uozo, dalili za uozo, dalili za uharibifu
Shadows of the curse	Dalili za laana, dalili za kulaaniwa

(Chanzo: Njia Salama)

Data katika Jedwali 7, iliorodhesha mifano ya polisemia. Katika safu ya LA dhana ilitajwa na visawe tafsiri kutolewa katika LP. Kwa mfano, neno *man*, visawe vyake vilikuwa *binadamu* na *kiume*. Katika LA, neno *man* linabainisha wazi kuwa ni binadamu wa kiume lakini katika LP, neno hilo halibainishwi kwani lilitafsiriwa kama binadamu na kiume. Matumizi ya neno *man* katika muktadha wa kidini, linarejelea jinsia zote, kike na kiume. Kwa hivyo, tafsiri ya neno *man*, ilikuwa tata kwa sababu ya kuwa na maana zaidi ya moja.

Pili, kirai *bright of decay* kilitafsiriwa kama *mianga ya uozo, dalili za uozo na dalili za uharibifu*. Mwisho, kirai *shadow of the curse* kilitafsiriwa kama *dalili za laana na dalili za kulaaniwa*. Matumizi ya polisemia katika tafsiri huwa changamoto kwa msomaji (Mohammed, 2009). Mohammed anaendelea kueleza kuwa tatizo hutokea wakati ambapo polisemia zimetumiwa katika sentensi zisizodhibitiwa na muktadha wa kiisimu ambao unaweza kuuondoa utata huo na kubainisha wazi maana inayorejelewa. Maalej (2015) anasema kuwa dhana ya polisemia ni ya kawaida katika lugha.

Maalej anafafanua kuwa dhana hizo za kiisimu husababisha matatizo katika tafsiri.

Kutoka na fafanuzi za wataalamu hao na data iliyotathminiwa, matokeo yalionyesha kwamba polisemia ni hali ambapo neno moja kuwa na maana zaidi ya moja. Pia, matumizi ya polisemia katika tafsiri yalisababisha matatizo ya kitafsiri.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Makala haya yalitathmini matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini za kidini: *Njia Salama, Walioteuliwa na Vita Kuu*. Uchunguzi huo ulithibitisha kuwepo kwa matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini teule za White. Matatizo ya kiisimu yalikuwa ya kisemantiki, kisintaksia na kimofolojia. Kwa upande mwingine, yale ya kimtindo yalikuwa ya urudiaji, uradidi na tofauti za polisemia.

Hali kadhalika, makala haya yalichambua na kueleza sababu za utokeaji wa matatizo ya kiisimu na kimtindo katika matini teule na yaligundua kuwa matatizo hayo yalitokana na uhamishwaji usiofaa wa maneno ya kijumla katika tafsiri,

haiponemia, maneno ya kimahusiano, maana msingi, rejelewa na dhanishi kutoka lugha asilia hadi lugha pokezi.

Aidha, utafiti huu uligundua kuwa matatizo ya kisintaksia yalikuwa ya njeo, uteuzi mbaya wa viambajengo katika sentensi, ukiushi wa miktadha katika kuhamisha ujumbe tafsiri, udondoshaji na uongezaji wa vipashio katika matini tafsiri, uhamishwaji usio makini wa maneno, virai na vishazi katika matini.

Isitoshe, ilibainisha kuwa matatizo ya kimofolojia yaliathiri uelewaji na ufasiri wa ujumbe tafsiri mwa waumini wa SDA. Baadhi ya matatizo hayo yalisababishwa na makosa ya kimaendeleo, unganishwaji na utenganishwaji wa maneno usiosahihi na uundwaji legevu wa maneno. Hatimaye, matatizo ya kimtindo yalisababishwa na tofauti za mitindo, miundo baina ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa hivyo, matatizo hayo yalikuwa urudijaji, uradidi na tofauti za kipolisemia.

Tathmini hii ilibainisha kuwepo kwa matatizo mengi ya kiisimu na kimtindo katika matini teule yaliyopelekea waumini wa SDA kusoma, kuelewa na kufasiri ujumbe tafsiri kwa njia tatanishi. Vilevile, uchambuzi wa matatizo hayo, uligundua kuwa mikakati na mbinu zilizotumiwa na wafasiri wa vitabu teule zilichangia kufanyika kwa matatizo katika matini tafsiri. Baadhi ya mikakati iliyotumiwa ilikuwa pamoja na tafsiri huru, tafsiri sisisi, mkopo wa moja kwa moja, ukopaji, udondoshaji, unukuzi, uyenyejishaji, ugenishaji na ufidiaji. Mikakati hiyo ilisababisha tafsiri finyu na pana katika matini hali ambayo iliwanyima wasomaji lengwa uelewaji na ufasiri wa kuaminika na kukubalika wa ujumbe tafsiri. Kwa hivyo, mapendekezo yafuatayo yanaweza kutekelezwa:

- Watafsiri wa matini za kidini wazingatie kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili wanapotafsiri ili kuepesha matatizo ya kiisimu na kimtindo katika tafsiri.
- Shughuli ya kutafsiri matini za kidini inahitaji uhariri wa hali ya juu kwa sababu ni matini

adilifu inayolenga kufahamisha hadhira ukweli wa matukio na mafunzo kwa uaminifu na ukubalifu.

- Matni tafsiri za Kiswahili yatafsiriwe upya kwa kuzingatia hadhira lengwa, tofauti kiisimu, kimtindo na kitamaduni za jamii husika

MAREJELEO

- Amorim, N. (1990). *Histoire de l'Englise. Adventiste. UAAC. Mundende, Rwanda. zake*", Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ali, S. M. (1965). *Matatizo na Matumizi ya Kutafsiri Sheria Swahili Dar-es-salam University Collage.*
- Boase-Beier, J. (2006). *Saying what someone else meant; style, relevance and translation International Journal of applied linguistics*14 (2); 276-86Cleve Don Multilingual matter LTD.
- Crystal, D. (1991). *A dictionary of linguistics and phonetics. 3rd edition.*
- Crystal D., 1987, *The Cambridge Encyclopedia of Language, Cambridge*
- Ghazala, H. (2008). *Translation as Problems and Solutions, Special Edition. Beirut: Dar Elilm lilimalayin.*
- Hartman, R.R.K. (1972). *Dictionary of language and linguistics. London: Applied Science.*
- Hervey, S., & Higgins, I. (2002). *Thinking Translation. London & New York: Routledge*
- Holz-Mänttari, J. (1984). *Translatorisches handeln: Theorie und method. Helsinki. Suomalainen Tiedeakatemia.*
- Leech, G. (1981). *Semantics. The Study of Meaning. Second edition revised and updated. Harmondsworth: Penguin Books.*

- Lyons, J. (1977). *Semantics*. Cambridge. Cambridge University Press.
- Kombo, D. K. & Tromp, D.L. (2006). *Proposal and Thesis Writing an Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Maalej, Z. (2015). On the role of Arabic in the misuse of English determination in Arab students written production. Kingdom of South Arabia. King Saul University.
- Mathew, P.H (1974). *Morphology*. Cambridge. Cambridge University Press.
- Massamba D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. TUKI, Dar es Salaam.
- Mathieu. (2003). Translation Studies. The Central Issues of Translation. Division.” Adventist World.
- Murundu, A.G. (2021). East Kenya Union Conference. Nairobi. East Central Africa.
- Mbwana, G. (2014) “Like a Mustard Seed: Adventism in East and Central Africa Division.” *Adventist World*.
- Munday, J. (2016). *Introducing translation studies. Theories and Applications*. London. Routledge.
- Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications*. Leiden. Routledge.
- Mwansoko, H.J.M. (1992). (mh) “The Style of Swahili Academic Writing,” *Katika M.P. Academic Writing: The State of Art*. Avon: Multilingual Matters Ltd.
- Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*. London: Prentice Hall.
- Nida, E.A. (2000). *Principles of correspondence*. In Laurence Venuti (ed.). *The translation studies reader*, 126-140. London: Routledge. (Original work published 1964).
- Nida, E.A. & Taber, C.R. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden. E. J. Brill,
- Nord, C. (2007). *Translating as a Purposeful Activity: Functionalist Approaches Explained*. Manchester. St. Jerome Publishing.
- Ochorokodi, J. (2021). West Kenya Union Conference. Kisumu. Kenya National Bureau of Statistics.
- Reiss, K. (1990). *Translation Criticism – the Potentials and Limitations*. London and New York. Taylor & Francis Group
- Reiss, K. & Vermeer, J. (1984). *Toward a general theory of translation action, skopos theory explained*. London & New York. Niemeyer.
- Schaffner, C. (1998). *Action (Theory of Translational action)*. In M. Baker, ed. *Routledge Encyclopedia of Translation Studies*. London. Routledge.
- Smith, C. (2022). *Souls in Transition: The Religious & Spiritual Lives of Emerging Adults*. Amazon. Oxford University Press.
- Snell-Hornby, M. (1995). *Translation studies – An integrated approach*, Revised Edition. Amsterdam. John Benjamins.
- TUKI (2012). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar Es salaam. Oxford University Press.
- TUKI (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- TUKI (2006). *English-Swahili Dictionary*. Dar es Salaam. TUKI.
- TUKI (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. TUKI
- Vermeer, H. J. (1984). *Towards a general theory of translational action. Skopos theory explained*. New York. St. Jerome. Publishing.
- Webster (1828). *American dictionary of the English language*. New York. Noah Writers Ltd.
- White, G.E. (2009). *Walioleuliwa*. USA. United Bible Society.

White, E. (1977). *Njia Salama*. Kisii. South Kenya Bookhouse.

White G. E. (1952). *Vita Kuu*. USA. United Bible Society...

Yang, W. (2010). *A tentative analysis of errors in language learning use*. Journal of language teaching and research. Vol 1.